

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

**KUWASILISHA MAOMBI YA USAJILI NA LESENI YA UFUGAJI WANYAMAPORI
KWA MWEZI JANUARI HADI MACHI, 2021**

Wizara ya Maliasili na Utalii inawajulisha wananchi wanaotaka kuanzisha miradi ya ufugaji wanyamapori katika Bustani (Zoo/Sanctuary), Mashamba (Farms/Breeding Sites) na Ranchi (Ranch) au kuanzisha Eneo la Wanyamapori Yatima (Wildlife Orphanage facility) kuwasilisha maombi yao kwa Kamishna wa Uhifadhi, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania. Mwombaji atatakiwa kujaza Fomu za Maombi ya Usajili na Leseni zinazopatikana kwenye ofisi za TAWA Makao Makuu Morogoro (Jengo la TAFORI), ofisi za Utalii na Huduma za Biashara, Dar es Salaam (Gorofa ya 4, Jengo la Mpingo) na ofisi ya Matumizi Endelevu ya Wanyamapori - Arusha zilizopo karibu na ofisi za jeshi la zima moto.

Hakuna Usajili au Leseni ya Daraja lolote itakayotolewa kwa madhumuni ya kuzalisha wanyamapori hai kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi.

Maombi ya Leseni za ufugaji ni kwa Madaraja yafuatayo:-

Daraja	Maelezo
17	Bustani ya Wanyamapori (Wildlife zoo & sanctuary)
18	Mashamba ya kufuga wanyamapori (Wildlife farms & breeding sites).
20	Ranchi za wanyamapori (Wildlife Ranch)

Mwombaji anatakiwa kuwasilisha fomu ya maombi ya leseni pamoja na viambatisho vifuatavyo:-

1. Uthibitisho wa umiliki wa ardhi itakayotumika kwa ajili ya mradi wa ufugaji wanyamapori,

2. Endapo mwombaji ni mtu binafsi anatakiwa awasilishe hati ya usajili wa jina la biashara (Certificate of Registration of Business name) au iwapo mwombaji ni kampuni awasilishe hati ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association),
3. Hati ya utambulisho wa mlipa kodi (Taxpayer Identification Number),
4. Uthibitisho kwamba biashara ina Leseni kutoka kwenye Mamlaka husika,
5. Mpango wa biashara [Business plan] unaohusu biashara inayotarajiwa kufanywa na uthibitisho wa kuwa na mtaji wa kufanya biashara hiyo,
6. Uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya usajili na leseni kama ilivyoainishwa hapo chini na ambayo haitarudishwa [Non- Refundable];
 - i. Bustani ya wanyamapori; ada ni TZS 30,000/= kwa mzawa na mzawa pamoja na Mgeni ni TZS 50,000/=
 - ii. Mashamba ya ufugaji wanyamapori; ada ni TZS 40,000/= kwa mzawa na kwa mzawa na mgeni ni TZS 100,000/=
 - iii. Ranchi ya wanyamapori ni TZS 100,000/= kwa mzawa na kwa mzawa na mgeni ni TZS 200,000/=
7. Mwombaji asiwe na rekodi ya kupatikana na hatia ya kuvunja Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

Imetolewa na.

**KAMISHNA WA UHIFADHI
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA,
Barabara ya Dar es Salaam,
Eneo la Kingolwira, Jengo la TAFORI,
S.L.P 2658,
MOROGORO
Simu: 023-2934204
Barua pepe: cc@tawa.go.tz**